Uumbaji

“Mungu ni Muumbaji wa vitu vyote, na amefunua katika Maandiko Matakatifu uhalisi wa tukio la utendaji wake wa uumbaji. Katika siku sita Bwana alifanya “mbingu nan chi” na vitu vyote vilivyo hai juu ya nchi, akastarehe siku ya saba ya juma lile la kwanza. Kwa hiyo akaanzisha Sabato kama kumbukumbu ya milele ya kukamilisha kazi yake ya uumbaji. Mwanamume na mwanamke wa kwanza waliumbwa kwa mfano wake Mungu kama upeo wa kazi yake ya Uumbaji, wakapewa utawala juu ya ulimwengu, na kuagizwa wajibu wa kuutunza. Wakati ulimwengu ulipomalizika kuumbwa, ulikuwa “(m)ema ukitangaza utukufu wa Mungu.” (Mwa.1:2, Kut.20:8-11; Zab.19:1-6; 33:6, 9; 104; Ebr. 11:3)

Maelezo ya Biblia ni rahisi. Kwa amri ya Mungu ya uumbaji, mbingu na nchi ambazo zilikuwa tupu, zilipata sayari iliyojawa viumbe hai vilivyokomaa na mimea kwa aina zake. Ndipo Mungu akapumzika kusherehekea uumbaji wake. Hebu tuangalie uumbaji ulikuwaje.

Mungu aliumba kwa siku sita. “Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu nan chi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji. Roho ya Mungu ikatutulia juu ya uso wa maji.” (Mwa.1:1, 2)

Siku ya *kwanza:* Aliumba nuru, akatenga nuru na giza na kuyapa majina (Mwa.1: 3, 4).
Siku ya *pili*: Mungu aliumba anga, akatenga maji yaliyo juu na yaliyo chini na kuyapa majina (Mwa.6-8).
Siku ya *tatu*: Mungu aliumba bahari. Pia akaotesha mimea kwenye nchi (Mwa.1:9-13)
Siku ya *nne*: Mungu aliumba mianga, akaipa kutawala usiku na mchana, akaumba na nyota pia. Mianga iliwekwa kuwa dalili ya majira, siku na miaka. (Mwa.1:14-19)
Siku ya *tano*: Mungu aliumba viumbe vya majini, nyangumi nk. Pia aliumba ndege wa angani (Mwa.1: 20-23)
Siku ya *sita* aliumba wanyama wa nchi kavu, vitambaavyo, wanyama wa mwitu. Pia kuwekea uumbaji taji, alimfanya mwanadamu mwanamume na mwanamke ili atawale (Mwa. 1:24-30). Baada ya uumbaji, Mungu aliona kuwa ni vema sana. (Mwa. 1: 31
Siku ya *saba*: Mungu alipumzika, akastarehe, akaibariki na kuitakasa (Mwa. 2:1-3)

Neno la Mungu liumbalo
Kwa neno la BWANA, mbingu zilifanyika (Zab.33:6). Je, neno lilitendaje kazi?

Neno Liumbalo na Maada iliyokuwapo
Maneno ya Mwanzo “Mungu akasema” huingiza amri yenye nguvu ya Mungu iliyowajibika kuumba. (Mwa.1:3, 6, 9, 11, 14, 20, 24). Kila amri ilikuwa na nguvu ya kuumba iliyobadili nchi iliyokuwa ukiwa na yenye utupu kuwa Paradiso. Maana yeye aliamuru, ikasimama (Zab.33:9). Maneno yalibuniwa na Neno la Mungu (Ebr.11:3). Maneno hayakutegemea kilichokuwako, kwa kuwa kwa vitu vinavyoonekana, vilifanywa kutokana na visivyo dhahiri (Ebr.11:3). Japokuwa kuna wakati Mungu aliumba kwa kutumia vinavyoonekana, Adamu na wanyama waliumbwa kutokana na udongo, Hawa aliumbwa kutoka kwenye ubavu wa Adamu, (Mwa.2:7, 19, 22), bado ni Mungu ndiye aliyeumba vyote.

Habari ya Uumbaji

Maswali mengi yameibuka kuhusiana na uumbaji. Je hakuna migongano kwenye uumbaji, au hivi ni kweli uumbaji ulikamilika miaka 6, 000 tu iliyopita na siyo vipindi virefu?

Maelezo ya Uumbaji. Biblia inayo maelezo ya aina mbili ya uumbaji. Ya kwanza ni Mwanzo 1:1- 2:3. Na ya pili yanaanza Mwanzo 2:4 – 25. Maelezo ya pili yanaanza "hivyo ndivyo vizazi vya mbingu nan chi zilipoumbwa" na kuunganisha historia ya uumbaji. (cf. Mwa.5:1; 6:9; 10:1).

Siku za Uumbaji. Siku ya uumbaji inafanya siku halisi ya saa 24. Ndivyo walivyohesabu siku, watu wa Mungu, kwa kuangalia jioni na asubuhi; (Mwa.1:5, 8, 13, 19, 23, 31) siku ikianza jioni na kwisha asubuhi (Law.23:32; Kumb.16:6). Neno siku (yom) linapofuatiwa na namba (Mfano. Mwa.7:1 na Kut.16:1) ina maana ya siku ya saa 24. Amri kumi hutoa ushahidi kuwa uumbaji ulikuwa wa siku sita tu. (Kut.20:8-11). Wale wanaotumia 2 Petro 3:8 kuwa siku moja ni sawa na miaka elfu, huacha kusema miaka elfu ni sawa na siku moja.

Mbingu ni kitu gani: Watu wengine hushangazwa, je, mbingu ni kitu gani? Je, Mungu aliumba jua, mwezi na nyota miaka 6,000 tu iliyopita? (Mwa.1:1; 1:14-19 cf. 2:1; Kut.20:11). Uumbaji wa mbingu na nchi haukusisha mbingu ambayo ilikuwa maskani ya Mungu. Tunaambiwa kuwa siku moja wana wa Mungu walikutana kwenye kona moja ya ulimwengu (Ayu. 1:6-12). Hivyo uumbaji wa Mwanzo 1 na 2 unaelekea kuwa wa jua na mfumo wake wa sayari.

Mungu wa Uumbaji

Mungu anayejali. Alipoanza kuumba, alianza na mazingira mazuri kwa ajili ya mwanadamu, kabla ya kumwumba mwanadamu.

Ni nani Mungu Muumbaji? Wote, Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu walihusika. (Mwa.1:1, 26.) Aliyekuwa mtendaji mkuu ni Mungu Mwana (Yoh.1:1-3; Kol.1:16;). Yesu ndiye aliyekuwa mwumbaji aliyeifanya dunia hii kuwako. (Efe.3:9; Ebr. 1:2, 3)

Onyesho la Upendo wa Mungu. Wakati anamfinyanga Adam, alijua mikono hiyo ndiyo itakayomsulubisha. Lakini bado alikubali kwa kuwa ni mwanakondoo aliyechinjwa kabla ya misingi ya ulimwengu. (Uf.13:8).

Makusudi ya Uumbaji

1. Kudhihirisha utukufu wa Mungu (Zab.19:1-4; Rum.1:20)
2. Kujaza nchi (Isa.45:8). Wakati mwanamume wa kwanza alipohitaji mwenzi, Mungu aliumba mwanamke (Mwa.2:20; 1Kor.11:9), hivyo akaanzisha ndoa ((Mwa.2:22-25). Mungu hakuwapa tu kutawala bali aliwaambia zaeni mkaijaze nchi (Mwa.1:28)

Umuhimu wa Uumbaji

1. Hukemea ibada ya sanamu (1Nya.16:24-27; Zab.96:5, 6; Isa.40:18-26; 42:5-9; 44)
2. Msingi wa ibada ya kweli (Zab.95:6, Ufu. 14:7)
3. Sabato, Ukumbusho wa uumbaji (Mwa.2:2-3; Kut.20:8-11; 31:13-17; Eze.20:20, 12)
4. Ndoa (Mwa.2:24;Mk. 10:9)
5. Msingi wa kujithamini (Kwa kuwa tuliumbwa katika sura ya Mungu Mwa.1:26, 27)

6. Msingi wa kuthaminiana (Kwa kuwa sisi sote Baba yetu ni Mungu Mal.2:10)
7. Uwakili wa mwili - tuwe na afya kimwili, kiakili, na kiroho (Mwa.1:29)
8. Kuwajibikia mazingira (Mwanaume na mwanamke waliwekwa bustanini Mwa.2:8 na walipewa kutawala wanyama wote. Mwa. 1:28)
9. Heshima ya kazi ya mikono (Mwa.2:15)
10. Thamani ya ulimwengu unaoonekana (Ni mwema Mwa.1:10, 12, 17, 21, 25). Alipomaliza, aliona ni njema sana (Mwa.1:31)
11. Suluhisho la shaka, upweke na kukosa maana (Mwa.1:26, 27)
12. Utakatifu wa Sheria ya Mungu (Mwa.2:17; 3:22-24)
13. Utakatifu wa maisha (Zab.139:13-16, Isa.44:24)

Kazi ya Uumbaji ya Mungu inaendelea

Je, Mungu amekamilisha uumbaji wake? Habari ya uumbaji inaisha kwa hoja kuwa "basi mbingu na nchi zikamalizika na jeshi lake lote" (Mwa.2:1). Agano Jipya linathibitisha kuwa kazi zile zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu (Ebr.4:3). Je, hii yaweza kumaanisha kuwa nguvu ya Kristo ya kuumba haitendi kazi? La hasha. Nguvu ya uumbaji ingali ikitenda kazi katika njia mbali mbali.

1. ***Kristo na Neno lake Liumbalo.*** Miaka 4,000 baada ya uumbaji, akida alimwambia Yesu, "sema neno tu na mtumishi wangu atapona" (Mt.8:8). Kama alivyosema wakati wa uumbaji, Yesu alisema na mtumishi akapona.

2. ***Neno liumbalo leo.*** Mungu ndiye anayeushikilia ulimwengu, ***"***akifunika mbingu kwa mawingu","akiitengenezea mvua nchi" na "huotesha majani milimani". Humpa mnyama chakula chake na wana kunguru waliao. (Zab.147:8, 9 cf. Ayu. 26;7-14). Huvishikilia vitu vyote kwa neno lake na vitu vyote hushikana katika yeye (Kol.1:17 cf. Ebr.1:3). Ndani yake tunaishi (Mdo.17:28)

   Uwezo wa Mungu wa kuumba huhusika pia katika kukomboa na kurejesha. Huumba upya mioyo yetu (Isa. 44:21-28; Zab.51:10). Tumeumbwa ili tutende mema (Efe.2:10) na kila aliye ndani ya Kristo ni kiumbe kipya (2Kor.5:17). Uwezo ule ule ulioumba mbingu na nchi, ndio utakaotumika kuumba mbingu mpya na nchi mpya (Isa.57:17-19; Uf.21, 22)

Uumbaji na Wokovu
Uumbaji na wokovu vinakutana katika Kristo Yesu.

Kipindi cha Uumbaji. Katika uumbaji, Kristo aliamuru na vikatokea mara moja. Kazi yote ilifanyika katika kipindi cha siku sita tu. Ingeweza kutoka hata siku moja; yaelekea alipendezwa kuthamini kuifunua sayari yetu kwa jinsi alivyofanya.

Yesu hakuamuru wokovu utokee. Mchakato wa kuokoa mwanadamu umetanda kwa karne nyingi. Umehusisha agano la kale na jipya, miaka 331/2 Yesu aliyoishi duniani, na karibu miaka 2000 akituombea mbinguni. Hapa kuna kipindi kirefu, karibu miaka 6000 na watu hawajerea kwenye bustani ya Edeni. Kuendelea kusubiri kwa Mungu katika mchakato wa wokovu huelezea nia yake ya kutaka kila moja aokolewe (2Pet.3:9)

Uwezo wa Kristo Kuumba. Eden, Yesu alisema uumbaji na Bethlehemu, mwumbaji akawa sehemu ya uumbaji. (Yoh.1:14). Huku ni kujishusha kwa namna gani! Hakuna aliyeshuhudia Kristo akiumba mbingu na nchi, lakini wengi walishuhudia uwezo uliofanya kipofu aone (Yoh.9:6, 7), bubu akaongea (Mt.9:32, 33), wakoma wakapona (Mt. 8: 2, 3), wafu wakapata kuishi tena (Yoh.11:14-45).

Kristo alikuja kama Adamu wa pili, mwanzo mpya wa uanadamu (Rum.5). Alimpa Mwanadamu mti wa uzima Edeni, mwanadamu akamtundika Yesu kwenye mti Kalvari. Paradiso mwanamu alisimama akiwa mrefu, akiwa katika sura ya Mungu, Kalvari, mwanadamu alining'inia kwenye mti akiwa mhalifu. Kwenye Ijumaa zote mbili, tamko lilitolewa "Imekwisha". (Mwa.2:2; Yoh.19:30), kuashiria kukamilika uumbaji na kukamilika ukombozi. Mkono wa Kristo ulifanya yote haya, uumbaji na ukombozi. Hivyo, tumeitwa kumtukuza Mungu katika maisha yetu.